# BODI YA KOROSHO TANZANIA

## TANGAZO KWA WADAU WOTE WA TASNIA YA KOROSHO NCHINI

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) inapenda kuwataarifu wadau wote wa Tasnia ya Korosho nchini kwamba Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe kwa kutumia Sheria Namba 18 ya mwaka 2009 ameongeza muda wa kibali cha kusafirisha korosho ghafi kwa muda wa saa 24. Ruhusa hii awali ilikuwa inaishia tarehe 15/11/2024 lakini kutokana na kuendelea kuwepo kwa mlundikano wa korosho kwenye ghala za Vyama vya Msingi katika baadhi ya maeneo muda wa kusafirisha korosho ghafi umeongezwa hadi tarehe 30/11/2024.

Aidha, ruhusa hii imeendelea kutolewa kwa korosho zinazosafirishwa kutoka ghala kuu zilizopo mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma kwenda Bandari ya Mtwara au katika ghala za kuhifadhi korosho zilizopo Mtwara, Pamoja na usafirishaji wa korosho ghafi kutoka kwenye Vyama vya Msingi (AMCOS) kwenda Ghala Kuu ambao utafanyika hadi saa nne (4) usiku. Korosho zinazosafirishwa kutoka maeneo mengine (Pwani na Morogoro) kwenda Bandari ya Dar es Salaam zitaendelea kusafirishwa kuanzia saa 12:00 Asubuhi hadi saa 12:00 jioni kama ilivyo katika Mwongozo Na.1 wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Korosho Ghafi kupitia Stakabadhi Ghalani Msimu 2024/2025.

Imetolewa na:

**MKURUGENZI MKUU**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**

**LEO TAREHE 11 NOVEMBA 2024**